**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI**


Simu Na. 028 2802535
Fax Na. 028 2802535

Unapojibu tafadhali taja:
**Kumb. L.20/67/110**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa
Halmashauri ya Manispaa,
S.L.P 44,
**KIGOMA.**
Tarehe: 17/2/2022


## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI NAFASI 400.

Napenda kukujulisha Umma kuwa Halmashairi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji inatekeleza maelekezo ya Serikali ya kuweka Mfumo wa Anuani za Makazi ambapo pamoja na mambo mengine utahusika na ukusanyaji wa taarifa za anwani za makazi katika Mitaa. Kwa sababu hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda ya kukusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Kata na Mitaa ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

### A. SIFA ZA WAOMBAJI

1. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35
2. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
3. Awe anamiliki simu janja (smartphone) yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa muda usiopungua masaa 12.
4. Awe na Barua pepe inayofanya kazi
5. Awe ana uwezo wa kusoma Ramani za Mitaa

### B. KAZI NA MAJUKUMU

a. Kugawa/kuandika namba za Nyumba,Viwanja na maeneo ya Huduma
b. Kukusanya taarifa za Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma
c. Kukusanya taarifa za wamiliki wa Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
d. Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi.
e. Kazi hii itafanyika kwa muda wa miezi 2

**C. MALIPO**

Malipo kwa mwezi ni shilingi 300,000/=, pia atalipwa kiasi cha shilingi elfu thelathini **(30,000)** kwa kila mwezi kama fedha ya Bando kwa ajili ya kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi.

**D. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA.**

i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha 3 (Passport Size)
iv. Barua ya maombi ipitishwe kwa Mtendaji wa Mtaa na Kata anayoishi

**E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI.**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **21/2/2022 saa 9:30 Alasiri**

MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA KIGOMA UJIJI
S.L.P 44
**KIGOMA**

Athumani F. Msabila
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**KIGOMA UJIJI**

MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGOMA/UJIJI